# Nafasi ya Mwingiliano Fani katika Kukuza Fasihi ya Watoto

*Ibrahim Matin*[1], *Caren Nyandiba*[1] *na Sangai Mohochi*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Rongo*
[2]*Chuo Kikuu cha Kibabii*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahusu jinsi vipengele vya fani vinavyotumiwa katika vitabu vya fasihi ya watoto ili kufanikisha malengo ya waandishi. Utafiti uliofanywa uliongozwa na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure (1916). Nadharia hii inajibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja kwa nyingine katika kufanya kitu kizima. Kwa kuongozwa na nadharia hii tulichukulia fasihi kuwa kitu kizima kinachojengwa kwa maudhui na fani. Katika ngazi ya pili fani nayo imeundwa kwa vipengele mbalimbali vya lugha kama vile methali, misemo, nahau, taswira, picha na tashbihi. Vipengele hivi vilitambuliwa na matumizi yavyo yakafafanuliwa na kuelezwa. Utafiti huu uliteua kimakusudi riwaya za *Kisasi Hapana, Nimefufuka, Sitaki Iwe Siri,* na *Wema wa Mwana* katika kuchunguza jinsi mwingiliano fani unavyofanikisha kazi za fasihi zinazolenga watoto.**

**Maneno Muhimu**: mwingiliano, fani, fasihi ya watoto, umuundo

## Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Waandishi wa fasihi husuka fani ili kuwateka wasomaji wao wanaposoma kazi walizoandikiwa wakiwa na lengo la kuwaathiri kimawazo huku wakiwaburudisha. Vigezo wanavyotumia ili kutimiza lengo lao ni kama vile uzito wa maudhui na uchangamani wa msuko. Kwa kufanya hivyo kazi ya fasihi inaweza kufumiwa ama watu wazima au watoto. Fasihi ya watoto huwa na upekee wa kimtindo, fani na hata wa kimaudhui. Wasanii wa fasihi ya watoto aghalabu hufuma kazi zao kwa kuhulutisha fani mbalimbali kwa njia inayofanikisha ung'amuzi wa yaliyomo, uibuaji wa hisia na uzidishaji wa athari kwa watoto ambao huwa hawajakomaa kiakili. Ili kutimiza lengo hili hubidi waandishi hawa kutumia mwingiliano fani unaohusisha picha na fani za kifasihi ili kujaribu kutoa wazo lilelile katika njia itakayokuwa rahisi kwao kusoma na kuelewa. Lengo hasa ni kuwafanya wazidi kufurahia kusoma na kupata maana kwa kubainisha na kujaliza uelewekaji wa maudhui na pia kusaidia katika kumbukizi za vitushi muhimu kwa watoto hawa. Ni kwa mkabala huu ambapo makala haya yanalenga kuainisha jinsi vipengele vya fani vinavyotumiwa katika fasihi ya watoto vinavyoingiliana katika kufanikisha

malengo ya waandishi. Makala haya yatajikita zaidi katika matumizi ya picha katika kuchangia vipengele vingine vya fani katika kukuza fasihi ya watoto.

## Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto inaweza kufafanuliwa kwa ujumla kuwa chochote kinachoweza kusomwa na watoto na kinaweza kuwa riwaya, ushairi, drama inayowalenga watoto au watu wadogo au wachanga kiumri. Pia tunaweza kueleza fasihi ya watoto kama sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaowahusu watoto. Kwa hivyo fasihi ya watoto ni sanaa maalum inayoandaliwa kwa ajili ya watoto na ambayo hadhira yake ni watoto. Inaweza pia kuwa fasihi ambayo msingi wake wa kidhamira huwarejelea watoto (Wamitila, 2003).

Maoni mengine kuhusu fasihi ya watoto yanahusu kuwahusisha watoto wenyewe katika kubuni kazi zao za fasihi. Kwa kuendeleza wazo hili Bakize (2014), anafasili fasihi ya watoto kama aina ya fasihi iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe na inahusu watu wa umri wa chini ya miaka 18. Kwa hivyo, jambo la msingi ni kwamba fasihi hii ni lazima iwe na dhamira rahisi na lugha yake pia iwe sahili na nyepesi kuelewa.

Kwa hivyo katika makala haya tunachukulia fasihi ya watoto kuwa ni sanaa itumiayo lugha sahili kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo na umri wa chini ya miaka 18. Ufafanuzi huu ulitusaidia kujiwekea mipaka kuhusu vitabu tulivyovitia ndani ya utafiti wetu na kuchunguzwa.

## Sifa za Fasihi ya Watoto

Katika kueleza sifa ambazo fasihi hii inapaswa kuwa nazo, Davies (1973) anasema fasihi ya watoto haina budi kuwa na wahusika mashujaa ambao ni watoto. Hii ni kwa sababu watoto wenyewe wanaweza kujinasibisha na mashujaa hao. Mashujaa hawa wanapaswa kuwakilishwa kupitia wahusika watoto. Maudhui yanapaswa kuwa mepesi na yasiyo na utata. Kiwango cha lugha kinafaa kuwa sahili na hata msamiati haufai kuwa mgumu. Sentensi zinafaa ziwe fupi na zenye kueleza ujumbe kwa uwazi. Matumizi ya mbinu rejeshi yanafaa kuepukwa kadri umri wa mtoto unavyozidi kuwa mdogo. Msamiati katika vitabu vya watoto unafaa uwe ambao unahusiana na uhalisi katika maisha ya kawaida. Inapaswa kuonyesha matendo na maisha ya mhusika kinaganaga, mhusika awe anatia hamasa na lazima fasihi hiyo iwe inaburudisha.

Fasihi ya mtoto sharti iwe na mhusika mkuu akiwa mtoto au kijana, dhamira iwe inayowahusu watoto, aidha lugha iwe sahili na iwe na mtazamo wa watoto kwa sababu mtazamo wao ni tofauti na ule wa watu wazima. Hivyo, ikiwa mwandishi ataandika kazi inayoendana na fikira za watoto basi atakuwa amefanikiwa kuiteka saikolojia yao. Kazi ya watoto inapaswa iwe na sentensi sahili na lugha rahisi inayoendana na hadhira ya watoto na mada itakayoteuliwa pia inapaswa kuwa inayoweza kuwavutia watoto. Baadhi ya mada zinazoweza kuwapendeza watoto ni

zile zinazosimulia juu ya jasura, safari, fantasia na kadhalika. Pia lazima kazi inayowalenga watoto iwe fupi na ya kiutendaji kwa sababu hadithi ndefu huwachosha na hivyo kupoteza mvuto kwao. Wahusika katika fasihi ya watoto kwa upande mwingine wanapaswa kuwa mchanganyiko wa wahusika wema na waovu na wahusika wanyama wapewe uhai kama wa binadamu kwani hali hii huwavutia sana watoto (Davies 1973, Wamitila, 2002).

Kazi za fasihi ya watoto sharti ziwe na michezo kwani watoto hupenda sana michezo. Fasihi hii ya watoto inapaswa kuwa na picha hasa za rangi, hili hufanya watoto kutosahau kwa urahisi na kuhusisha matukio katika hadithi na ulimwengu halisi (Bakize, 2014). Bakize anasisitiza kuwa mwega wa fasihi ya watoto kidhamira ni watoto wenyewe, huwa na lugha nyepesi, huwa na picha na michoro, zenye motifu ya safari, huwa fupi, huwa na wahusika bapa, wahusika wakuu huishia katika ushindi, zina muundo sahili, huwa na mwingiliano tanzu na pia huwa na mambo ya kifantasia. Ni muhimu pia fasihi hii kuwa na taharuki na fantasia kwa sababu fantasia huleta mvuto wa pekee na kuwafanya kufurahia sana (Pearson, 2012).

Msuko wa fasihi ya watoto unafaa kuwa mwepesi ili kumwezesha mtoto kufuata matukio yenyewe, maandishi huwa makubwa yanayoweza kuonekana, maandishi hutiwa rangi ili yavutie macho ya watoto, kuvuta makini na kuwachochea kusoma kazi teule (Wamalwa, 2015). Fasihi hii pia huwa na lugha rahisi inayoendana na hadhira ya watoto, aghalabu fasihi hii huhusiana na tungo fupi, husheheni vielelezo, picha au michoro yenye rangi, hutumia wahusika wakuu watoto na wahusika wanyama wanaozungumza na kutenda kama wanadamu (Vuuren, 1994).

## Umuhimu wa Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ina mchango mkubwa katika makuzi ya watoto kama wanavyosema Odaga (1985) na Norton (2010), kuwa fasihi ya watoto, kama ilivyo fasihi ya watu wazima, ni muhimu kwao kwani huwasaidia watoto kutamalaki hulka nzuri na kuwaepusha na tabia mbaya, humpatia mtoto nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu kazi fulani ya fasihi na hivyo kukuza uwezo wake wa kiakili. Aidha humpatia mtoto nafasi ya kujua utamaduni wa jamii yake na ule wa jamii nyingine na hivyo kuboresha mtagusano. Fasihi hii pia huwapatia watoto nafasi ya kukua katika uwezo wao wa kihisia na kimaadili, husaidia mtoto kuwa mbunifu, kukuza utu wake binafsi na kisha kumsaidia kukuza utamaduni wa kusoma.

Hunt (1994), anaongezea kwa kusema kuwa dhima ya fasihi ya watoto ni kupitisha muda, kupata elimu, kupanua uwezo wa kufikiri, kurithisha tamaduni na maadili ya jamii, kupambana na masuala kadhaa na matatizo mbalimbali kama magonjwa na kadhalika. Kwa upande wake, Ngugi (2011), anaorodhesha baadhi ya dhima ya fasihi ya watoto kama kujiburudisha, kujiondoa katika hali fulani ya matatizo anayopitia mtoto, kuchachawisha ubunifu, kusaidia watoto kujielewa na kuwaelewa watu wengine mbali na kupata uzoefu wa kuelewa umbo la lugha. Kwa

njia hiyo mtoto hupata maonyo, mawaidha, makatazo na maelekezo. Fasihi hii pia huendeleza utamaduni kwa kueneza au kuwarithisha watoto mambo yanayothaminiwa na jamii ili wayaendeleze na kuyahifadhi, kama vile kudumisha mila za kijamii.

Ili kufikia malengo haya waandishi wa fasihi ya watoto hujikakamua kuiandaa fasihi hii kwa namna inayomwezesha mtoto kuielewa mwenyewe bila ya kumhusisha mwingine. Hili humsaidia mtoto kuelewa ulimwengu wake na kupata mafunzo kutokana na kazi husika. Njia mojawapo wanayotumia kufikia lengo hili ni mwingiliano fani. Katika mbinu hii ya mwingiliano fani waandishi huhusisha fani zaidi ya moja kwa wakati mmoja ili kutokeza wazo fulani. Katika makala haya tutaonyesha jinsi picha imetumiwa kuchangia vipengele vingine vya fani kama tashbihi, misemo, nahau, methali na taswira ili kusisitiza maana na hivyo kuchangia maudhui. Kwa kufanya hivi makala haya yanachangia katika makuzi ya fasihi ya watoto.

**Mbinu za Utafiti**

Makala haya yalitokana na utafiti wa uchanganuzi matini na ulifanywa maktabani. Kupitia kwa njia hii ya uchanganuzi matini mambo yaliyohusika yalikuwa ni kusoma kwa undani vitabu tulivyoteua, magazeti, matini, makala, tasnifu, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizomo maktabani na mtandaoni na hivyo tukapata habari za kina (Kothari, 2008). Idadi jumla ya utafiti wetu ilikuwa ni vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa katika kufundisha watoto walio katika shule za msingi nchini Kenya. Fasihi hii inatia ndani mashairi, tamthilia na hata riwaya. Idadi kamili ya vitabu hivi haijulikani kwa uhakika. Kwa mujibu wa makala haya tulichunguza riwaya pekee kwa kuwa ilikuwa ni vigumu kutafiti vitabu vyote vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunza fasihi katika shule za msingi nchini Kenya. Kwa hivyo tuliteua riwaya zinazotumiwa kufundisha fasihi katika shule za msingi nchini Kenya na zimeandikwa na waandishi wanaume na wanawake. Kwa kuongozwa na vigezo hivi tuliteua kimakusudi riwaya nne za *Kisasi Hapana* (2008) iliyoandikwa na Ken Walibora, *Nimefufuka* (2011) iliyoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* (2008) iliyoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* (2012) iliyoandikwa na Nuhu Bakari. Gall na wenziwe (1996) wanashikilia kuwa mbinu ya uteuzi sampuli kimakusudi humwezesha mtafiti kuteua sampuli ambayo ina data ya kutosha, inayofaa utafiti na inayohitajika hasa katika utafiti wa kithamano. Mbinu hii pia humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayomwezesha kujibu maswali ya utafiti na anayoweza kumudu kiutafiti (Neuman, 2006).

Tulikusanya data kwa kusoma riwaya tulizoteua na kutambua data iliyooana na madhumuni ya makala haya kwa kudondoa vipengele vya fani; picha, nahau, methali, taswira na tashbihi. Katika uchanganuzi wa data tuliorodhesha vipengele vya fani tulivyopata kulingana na utokeaji wake na idadi kutoka kwa kila kitabu. Hatua ya pili ilikuwa ni kuchuja data tuliyopata kwa kuchagua vipengele vya fani tulivyokuwa tumeamua kuchunguza. Vipengele hivyo ni tashbihi, taswira, misemo,

nahau, methali na picha. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuchanganua vipengele vya fani kwa kina ili kuonyesha waziwazi jinsi kila kipengele cha fani tulichokuwa tumetambua kilivyoingiliana na picha. Katika hatua ya nne tulitoa ufafanuzi kuhusu jinsi vipengele hivyo vya fani vilivyofanikiwa kuchangiana ili kuleta maana iliyokusudiwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya umuundo na malengo ya makala haya. Tuliwasilisha data ya mwisho kithamano kwa kuzingatia maoni ya Truex (1996) ambaye anaeleza kuwa uchanganuzi matini kithamano humpa mtafiti nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele vya uumbaji wa sanaa na maana inayojitokeza katika vipengele vya sanaa hiyo. Katika muktadha huu vipengele vya uumbaji wa sanaa ni fani ambazo huchangiana ili kutokeza maana inayolengwa na mwandishi. Kwa hivyo tulionyesha jinsi fani mbalimbali zinavyoingiliana na picha ili kuleta maana inayokusudiwa.

## Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure (1916). Nadharia hii inajibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja kwa nyingine katika kufanya kitu kizima. Kwa kuongozwa na nadharia hii tulichukulia fasihi kuwa kitu kizima kinachojengwa kwa maudhui na fani. Katika ngazi ya pili fani nayo imeundwa kwa vipengele mbalimbali vya lugha kama vile methali, misemo, nahau, taswira, picha na tashbihi. Vipengele hivi vilitambuliwa na matumizi yavyo yakafafanuliwa na kuelezwa. Tuliongozwa na mihimili mitatu ya nadharia hii ya Umuundo katika makala haya. Kwanza kulingana na nadharia hii tukitaka kupata maana mwafaka ya kazi ya fasihi ni lazima tuchunguze muundo wake wa ndani, yaani mfumo wake wa lugha. Kulingana na mhimili huu, kuangalia fani moja kivyake ni kama kuiona kijujuu tu. Kwa hivyo tuliongozwa na mhimili huu ili kuhakiki picha inavyochangia vipengele vingine vya fani kama tashbihi, misemo, methali, taswira na nahau.

Pili, nadharia ya umuundo inashikilia kuwa katika kupata maana lazima kuwe na uhusiano wa kipembe tatu yaani dhana, alama na kitajwa. Kama vile muundo wa lugha ulivyo mfumo, muundo wa fasihi pia una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Katika kazi ya fasihi kuna kitengo cha sanaa kama vile maudhui, ploti, wahusika, muktadha na lugha. Hakuna kipengele cha fasihi kati ya hivi kitakachoelezwa katika upekee wake bali lazima kielezwe kwa kuzingatia kuwepo kwa jukumu la vipengele vingine kwa sababu vipengele hivi hushirikiana ili kujengana na kukamilishana na kuwa kitu kizima. Katika utafiti wetu tumetumia mhimili huu kuonyesha kuwa vipengele mbalimbali vya fani vinachangiana na kuwa ushirikiano uliopo baina ya vipengele hivi na unaovikamilisha unaweza kuchunguzwa. Pia tuliongozwa na mhimili huu kutathmini na kuchanganua data kwa kuchunguza ni vipi msanii husuka vipengele vya fani kama tashbihi, misemo, methali, taswira na nahau kwa kuvioanisha na picha ili kuleta maana kamili katika fasihi ya watoto.

Hatimaye nadharia hii ya umuundo husisitiza jinsi vipengele vya kazi ya sanaa

vinavyohusiana na kufungamana hadi kuikamilisha kazi hiyo. Sehemu hizo mbalimbali pia huweza kutenganishwa na kuchunguzwa. Kwa kuongozwa na mhimili huu tulitenganisha na kueleza vipengele vya fani kama tashbihi, misemo, nahau, methali na taswira na kuvichunguza. Kisha katika hatua ya pili tulionyesha jinsi vipengele hivi vinavyochangiwa na picha ili kutoa maana zaidi na hivyo kusaidia msomaji kuelewa na kukumbuka habari.

**Fani Katika Fasihi ya Watoto**

Fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake. Lugha anayotumia mwandishi huwa na sifa fulani, kwa mfano ina vikolezo au vitia ladha fulani na imesheheni au kujaza mbinu za kila aina (Wamitila, 2011). Kwa upande wake, Mbatia (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Pili ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya. Fani pia huweza kufafanuliwa kuwa ni mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo na maudhui. Mtindo huu bila shaka unaweza kutia ndani kiasi cha maandishi, urefu wa sura ya kitabu cha fasihi, picha na michoro (Wamitila, 2003).

Wamitila (2011) anaorodhesha vipengele muhimu vya fani kama muundo, mtindo, mandhari, mtiririko, matumizi ya lugha, picha, wahusika na uhusika. Anazidi kueleza kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu ya kazi ya fasihi na kuwa dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia wasomaji bila ya kuwako kwa lugha. Anasema kuwa katika uchunguzi wa lugha mambo yanayochunguzwa ni tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno, sajili za lugha, matumizi ya nahau na misemo mbalimbali. Mtaalamu huyu anapiga hatua na kueleza kuwa tamathali ya usemi ni neno au kifungu ambacho kina maana iliyofichwa. Tamathali hizi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, kuwa na msisitizo na mnato mkubwa. Baadhi ya tamathali hizi ni tashbihi, sitiari, tasfida, tashihisi, chuku, kinaya, dhihaka, maswali balagha na tabaini. Kwa upande wake, Mulokozi (1989) anaeleza tamathali za usemi kama tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya jamii. Tamathali za usemi zinapotumiwa katika kazi ya fasihi huibusha taswira mbalimbali katika akili ya msomaji na kumwezesha kuelewa ujumbe kikamilifu. Tamathali hizi ambazo ni vipengele vya fani ni kana vile tashbihi, sitiari, tashihisi, taniaba, taashira, majazi, lakabu, tabaini, tashtiti, tanakali za sauti, chuku, kinaya, dhihaka, methali, nahau, misemo, taswira, taharuki, mvutano na kadhalika (Njagi, 2002).

Mbinu hizi huteuliwa kulingana na hadhira inayolengwa na ujumbe unaokusudiwa kupitishwa. Ndipo Wamitila (2011) anasema kuwa ikiwa mwandishi anataka kumshawishi na kumwathiri msomaji wake ipasavyo, lazima ateue lugha yenye uwezo wa kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo mbinu zitakazotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa watoto huwa zile zinazowafaa kwa sababu mwandishi hulazimika kuziteua kimakusudi ili kuwafikishia ujumbe. Katika makala haya

vipengele vya fani vilivyojitokeza katika utafiti wetu ni pamoja na tashbihi, misemo, picha, nahau, methali na taswira. Katika sehemu inayofuata tutajadili vipengele hivi kwa kuonesha jinsi vinavyoingiliana na picha.

## Picha Katika Fasihi ya Watoto

Picha ni mbinu ya kupitisha ujumbe kwa picha, michoro au vielelezo. Picha zinapotumiwa hufanya kitabu kivutie kwa mtoto na kufanya iwe rahisi kwa mtoto kuelewa mambo makuu yaliyomo kitabuni. Kwa hivyo mchoraji wa picha katika vitabu vya watoto anapaswa kuwa mbunifu, makini na mwenye tajriba au ustadi utakaomwezesha kuchora michoro inayowavutia watoto wanaposoma (Cass, 1967). Anaendelea kusema kuwa picha zinapaswa kuwa za rangi zinazong'aa kama vile rangi nyekundu, manjano, kijani kibichi na kadhalika. Jambo la msingi katika matumizi ya picha na michoro ni kuwa huvutia msomaji hasa mtoto na hivyo husoma maandishi akiihusisha na michoro hiyo. Pia michoro hii hushikilia makini ya mtoto. Kutokana na maoni haya ni wazi kuwa picha ni kipengele muhimu cha fani katika fasihi ya watoto. Mawazo haya yanaungwa mkono na Bakize (2014), anayesema kuwa matumizi ya picha au michoro huonyesha uhalisia wa jambo linalosimuliwa na linaloendelea. Anaendelea kusema kuwa michoro na picha husaidia kueleza zaidi kile kinachozungumziwa katika kazi husika kwani huwa na mahusiano ya moja kwa moja na kile anachokieleza mwandishi au mtunzi. Hii ndiyo sababu picha zote kwenye riwaya za watoto zina rangi za kuvutia ili kuchochea hamu ya watoto, pia zinaeleweka kwa urahisi na hivyo huwa rahisi kwao kupata maana. Rangi na urahisi wa kueleweka pia hufanya watoto hawa kukumbuka mawazo makuu yanayoendelezwa katika kazi husika.

## Mwingiliano wa Picha na Vipengele Vingine vya Fani katika Fasihi ya Watoto

Mwingiliano fani ni pale ambapo kipengele kimoja cha fani kinaingiliwa na kipengele kingine cha fani au kipengele kimoja cha fani kutegemea kipengele kingine ili kupata maana kamili. Mwandishi huweza kutumia kipengele cha fani na kisha kuingiza kipengele kingine ili kukazia maana au kutokeza wazo fulani wazi zaidi. Katika makala haya tunachunguza jinsi waandishi wa fasihi ya watoto wanatumia vipengele vya fani kama tashbihi, nahau, taswira, methali na misemo na kisha chini ya kipengele hicho wanaweka picha au kwenye ukurasa huo huo wanaweka picha inayodokeza jambo lililosisitizwa na kipengele fulani cha fani.

Katika kuonyesha jinsi picha zinavyoingiliana na vipengele vingine vya fani kama vile tashbihi, nahau, methali, taswira na misemo, tulichanganua vitabu vya *Kisasi Hapana* (2008) kilichoandikwa na Ken Walibora, *Nimefufuka* (2011) kilichoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* (2008) kilichoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* (2012) kilichoandikwa na Nuhu Bakari. Kwa mujibu wa utafiti wetu, idadi ya picha zilizojitokeza katika vitabu hivi ni 52 kama ilivyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1: Idadi ya Picha Zilizotumiwa katika Vitabu**

| **Kitabu** | **Picha** |
|---|---|
| *Sitaki Iwe Siri* | 14 |
| *Nimefufuka* | 14 |
| *Wema wa Mwana* | 12 |
| *Kisasi Hapana* | 12 |
| **Jumla** | **52** |

Kutokana na data hii ni wazi kuwa waandishi hawa wametumia picha kwa kiasi kikubwa kwani wote kwa pamoja wametumia picha 52. Riwaya za *Sitaki Iwe Siri* na *Nimefufuka* zimetumia picha 14 kila moja huku *Wema wa Mwana* na *Kisasi Hapana* zikiwa na 12 kila moja. Kiasi hiki kikubwa cha picha katika kila kitabu ni thibitisho tosha kuwa picha ni kipengele muhimu cha fani katika fasihi ya watoto tofauti na fasihi ya watu wazima ambayo huwa na picha chache au hata moja tu kwenye jalada. Katika riwaya tulizohakiki pia ilibainika wazi kuwa kulikuwa na vipengele vingine vya fani kama vile tashbihi, nahau, taswira, methali na misemo ambavyo vilikuwa vimetumiwa kwa wingi. Vipengele hivi vimetumiwa kwa njia ya kwamba vinaingiliana na kipengele cha picha ili kukuza maudhui yanayohusika.

## Picha na Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia wazi. Tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungio vifuatavyo: kama, mfano wa, mithili ya, ja, kama vile, sawa na miongoni mwa vingine. Pia huweza kuelezwa kuwa ulinganisho wa moja kwa moja na ulinganisho huo unadhamiriwa kusisitiza sifa fulani akilini (Wamitila, 2003, 2011). Msokile (1992), kwa upande wake, anasema kuwa tashbihi ni tamathali inayotumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi ja, mithili ya, sawa na, mfano wa, na kama. Anaendelea kusema kuwa mtunzi hutumia ulinganisho huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi (Senkoro 2011). Kutokana na maoni ya wataalamu hawa ni wazi kuwa tashbihi hulinganisha watu au vitu kwa kutumia vilinganishi.

Katika mjadala huu tunaangazia jinsi waandishi wa fasihi ya watoto wanatumia picha pamoja na tashbihi katika kazi zao ili kusisitiza ujumbe wao kwa hadhira yao. Kwa mfano katika ukurasa wa 30 wa *Sitaki Iwe Siri* kuna maelezo yasemayo:

> Utingo mwanamume mwenye umri wa makamo hivi na mwenye macho mekundu kama damu… Kinywani alikuwa na miraa ambayo alikuwa anatafuna mithili ya mbuzi anayecheua nyasi… Katika mkono huo huo alifumbata furushi la miraa ambalo alikuwa anachovya na kutia kinywani na kuisagasaga kwa meno kama kinu cha mahindi… kondakta alisema huku akiligonga gari kwa mkono wake ulioonekana kukauka kama kibanzi cha ukuni. (Uku 30)

Baada ya maelezo haya mwandishi ametuwekea picha katika ukurasa huo inayoonesha abiria wakishuka kutoka kwenye gari. Katika picha hii pia kuna kondakta au utingo ambaye anafafanuliwa katika tashbihi tuliyotaja. Ni wazi kuwa lengo la picha hii ni kusisitiza maelezo haya.





**Picha 1: Utingo - *Sitaki Iwe Siri* (Ukurasa 30)**

Katika picha hii mwandishi anatuchorea picha kuonyesha jinsi kondakta huyu anavyoonekana. Ingawa hatuwezi kuona macho yake ili kubaini wekundu wake, tunaweza kuona jinsi mkono wake ulivyokauka na umebeba kiasi fulani cha pesa alizokusanya kutoka kwa wateja wake. Kukauka kwa mikono yake na wekundu wa macho unadokeza jinsi kazi hii ilivyo ngumu.

Pia katika ukurasa wa 3 wa *Sitaki Iwe Siri* tunaambiawa na mwandishi kuwa:

> Musa aliwaamsha kwa kuwatikisa kwa kuwa Haki na Ukwa walikuwa wazito wa usingizi. Walikuwa wamekwamilia blanketi kama siafu waliokwamilia nyama. Hivyo ilibidi Musa ajitahidi kwelikweli kuwaamsha. (Uku 3)

Kisha baada ya maelezo haya kwa kutumia tashbihi kuna picha inayodhihirisha wazo hili katika ukurasa huo huo. Picha hii inaonesha wazi jinsi Haki na Ukwa wameshikilia blanketi yao na ni kama hawasikii Musa anapoingia chumbani hata kwa kuwaita hadi inabidi Musa kuwashika na kuwatikisa ili waamke wajiandae kwenda shuleni. Hili linadokeza jinsi watoto wadogo wanavyopenda na kuthamini usingizi kwelikweli.



**Picha 2: Musa Akiwaamsha Dada Zake Haki na Ukwa *Sitaki Iwe Siri* (Ukurasa 3 )**

Katika ukurasa wa 5 Haki anamwambia Musa:

> Hujachana nywele aisee. Zinaonekana kama za mwendawazimu. (Uku 5)

Ili kusisitiza ujumbe huu mwandishi ameweka picha kando ya maelezo haya. Kwa njia hii ujumbe unakuwa wazi zaidi kwa msomaji.



**Picha 3: Picha ya Musa, Haki na Ukwa. Musa Anaonekana Akiwa na Nywele Ambazo Hazijachanwa - *Sitaki Iwe Siri* (Ukurasa 5)**

Katika picha hii ni wazi kuwa Musa hajachana nywele zake na kwa sababu hii mmoja wa dada zake anaonekana akimfanyia mzaha kwani haonekani vizuri akiwa mwanafunzi. Hata hivyo kulinganisha hali hii ya kutochana nywele na kuwa kama mwendawazimu ni kupiga chuku. Kwa njia hii jambo hili linasisitizwa na kukumbukwa kwa urahisi na mtoto. Kutokana na mifano hii imebainika kuwa waandishi wa riwaya hizi wametumia tashbihi pamoja na picha ili kutoa ujumbe kwa njia ya wazi zaidi na inayoweza kukumbukwa kwa muda mrefu na mtoto.

**Picha na Misemo**

Misemo ni hali ya kutumia maneno ya kawaida kinjozi au kwa njia isiyo ya kawaida na huhitaji mtu kufikiria kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Lengo la kutumia misemo ni kusitiri maana na kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo. Wamitila (2003) anasema kuwa msemo ni dhana inayotumiwa kuelezea tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi ili litolewe maadili au maonyo fulani. Lengo la misemo huwa ni kulinganisha maisha na matukio au vitu na pia kueleza kauli ambazo hueleza ukweli fulani. Misemo hutumika kutambulisha mazingira maalum au kujulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa kwa sababu maneno hayo hutumika kama yalivyo katika mazingira mahsusi kuleta maana maalum (Njagi, 2002). Katika fasihi ya watoto hasa katika riwaya tulizochunguza imebainika wazi kuwa kuna mwingiliano fani pale ambapo misemo imetumiwa sambamba na picha ili kuonesha wazi somo la kipengele cha misemo. Kwa mfano katika *Nimefufuka* kwenye ukurasa wa 17 kuna msemo:

> "Maisha ni safari ndefu, safari ya kupanda na kushuka." (Uku 17)

Kisha chini yake kuna picha inayoonyesha msichana fulani akikwea mlima ili kuweka jambo hili la ugumu wa kupanda mlima wazi kwa kuonyesha jinsi kuna mlima mkali uliojaa mawe na utelezi. Aidha, picha huongeza mambo mengine ambayo hayajatokezwa wazi zaidi katika msemo wala maelezo yaliyotumiwa. Kwa kutumia picha pamoja na misemo kwa njia hii mtoto anabaki akishangaa jinsi itakavyokuwa vigumu zaidi kwa msichana huyu kushuka baada ya kufika kilele cha mlima. Kwa njia hii somo linakuwa wazi zaidi kwa mtoto msomaji kuwa maisha ni magumu na mtu anahitaji kuwa mwangalifu na kujitahidi zaidi. Kwa kufanya hivi mtoto anafurahia usomaji wake na kumfanya kutaka kuendelea kusoma.




**Picha 4: Mkwea Mlima - *Nimefufuka* (Ukurasa 17)**

## Picha na Nahau

Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida. Aghalabu nahau huwa imesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno ya nahau yenyewe (Msokile, 1992). Nahau pia inaweza kufafanuliwa kuwa semi fupifupi ambazo hutumia lugha au maneno ya kawaida lakini hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno awali. Japokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida, kauli yake ina undani kiasi kwamba kwa wageni wasiofahamu lugha hiyo hawawezi kuelewa maana (Saluhaya, 2013). Namanya (2015) naye anaonelea kuwa nahau ni semi zenye kitenzi, tofauti na misemo ambayo ni semi zisizokuwa na vitenzi. Anaongezea kuwa nahau ina sifa kama kuwa na maana zaidi ya moja, huundwa kwa lugha ya mkato, nahau mbili au zaidi huweza kuwa na maana moja na pia huundwa kwa maneno mawili au zaidi. Dhima ya nahau katika jamii ni pamoja na kufunza maadili, kuhekimisha, kuendeleza utamaduni, kuleta matumaini na kukuza lugha. Wamitila (2003) anaongezea kwa kuweka wazi kuwa kimuundo nahau huwa na kitenzi na jina.

Katika riwaya za watoto imedhihirika wazi kuwa waandishi wametumia picha sambamba na nahau wakiwa na lengo la kutia ladha maana na kunogeza uelewa kwa hadhira yao. Kwa mfano katika *Nimefufuka* kwenye ukurasa wa 7 mwandishi anatumia nahau na anatueleza kuwa:

> Waganga na waganguzi walijitahidi kumtibu (Lena). Kuna waliochoma magome, wengine mizizi na majani na wengine wakapiga dua imponye lakini miungu wakakinai. (Uku 7)

Kisha baada ya maelezo haya mwandishi anatumia picha kuonyesha hili waziwazi ambapo kuna picha kwenye ukurasa huohuo ikionyesha waganga wawili na zana zao wakijaribu kutegua kitendawili cha ugonjwa wa Lena huku mama yake ameketi

kwa majonzi makubwa akisubiri kitendawili kiteguliwe. Kwa hivyo maelezo ya mwandishi yanajalizwa na picha ili habari hizi ziingie watoto akilini kwa urahisi.



**Picha 5: Mama ya Lena Akiwa kwa Mganga - *Nimefufuka* (Ukurasa 7)**

Kutokana na matumizi ya picha baada ya nahau, mwandishi anafafanua nahau kwa kutumia picha kwa maneno rahisi ili mtoto aweze kuelewa kuwa mama Lena alifanya bidii kutafuta suluhisho kwa ajili ya ugonjwa wa Lena lakini haikuwezekana. Waganga wanapiga dua kwa lengo la kuomba miungu waingilie kati na kutambua shida ya Lena ili angalau apate afueni.

Aidha katika ukurasa wa 4 katika *Nimefufuka* mama ya Lena anamwomba Musa amsindikize kutafuta Lena. Na mwandishi anasema:

> “Musa alisalimu amri.” (Uku 4)

Kisha, kuna picha inayoonyesha Musa akiwa katika sare yake ya kazi ameandamana na Mama Lena kuenda kumtafuta Lena alikopotelea. Picha hii inamwonyesha Musa kuwa alikuwa kazini na inabidi atoke asaidie mwenzake katika jitihada zake za kutafuta mwana wake aliyepotea. Kuwa kwa Musa na sare ya kazi ni dhihirisho tosha kuwa aliandamana na mama Lena shingo upande kwani hakuwa amepanga kufunga safari kama hii kwa wakati huu. Inambidi tu kufanya hivi kwa kutimiza wajibu.




**Picha 6: Musa na Mama Lena - *Nimefufuka* (Ukurasa 4)**

Kwa hivyo picha hii ambapo Musa ametoka akiwa katika sare yake ya kazi inajaliza nahau kwa kuonyesha kuwa ilimbidi Musa kutoka kwa dharura ili amsindikize mama Lena ili kutafuta mwanawe.

### Picha na Methali

Kwa ujumla methali inaweza kuchukuliwa kuwa ni aina ya usemi wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa wa kweli na unaotumika kufumbia au kutolea mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Methali ni aina ya semi inayotumiwa kuelezea kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili kitoe maadili au maonyo fulani (Njagi, 2002). Kulingana na Njagi (keshatajwa), methali humwingiza msikilizaji au msomaji katika hali ya kufikiri, kuchambua na kupatanisha ukweli na hali ili ajue maana ya ndani iliyokusudiwa, husaidia hadhira kukumbuka wazo kuu, hutumiwa kufafanulia maelezo ya msingi, kudhibiti kaida za kisarufi, hujenga taharuki, ni chombo cha kuwasilisha hisia, kubainisha itikadi za mtunzi, kuelekeza na kuadilisha jamii.

Kulingana na TUKI (2004), methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa. Senkoro (2011) kwa upande wake anaeleza methali kuwa ni kauli fupifupi zinazobeba uzoefu wa jamii kuhusu maisha na hivyo kuadilisha na kuhekimisha jamii. Kwa hivyo methali hubeba falsafa ya maisha ya jamii na hivyo hutumiwa kupitisha maadili kwa jamii husika.

Katika riwaya za watoto, waandishi wametumia methali sambamba na picha. Kwa mfano katika *Nimefufuka* mwandishi anatujuza katika ukurasa wa 22 kuwa:

> Ukosefu wa maadili katika jamii umechangia pakubwa kueneza matumizi ya vileo, tena vikali na maradhi hatari yakiwemo ya UKIMWI. Watu wafisadi maarufu katika jamii wanashiriki katika biashara haramu ya pombe na dawa za kulevya. Wanasahau kuwa mtego uo huo unawashika waliomo na wasiokuwamo. Na kama afanyavyo panya, mtu asiye na tahadhari atapita karibu na huo mtego na punde si punde kama smaku, kile chambo katika mtego kitamvuta na atajikuta amenaswa. (Uku 22)

Baada ya maelezo haya mwandishi ameongezea picha ya watu wakiwa barabarani wakiongea na ni kama hawana habari kuhusu hatari wanayoelekea kukabiliana nayo.



**Picha 7: Mtego Ulio Katikati mwa Barabara - *Nimefufuka* (Ukurasa 22)**

Kwa kutumia picha hii baada tu ya kutaja methali inakuwa rahisi kwa mtoto kuelewa kuwa mtego unaweza kunasa yeyote asipojihadhari na hili linakuwa somo na tahadhari kwake kuwa lazima kuwa macho na mwangalifu kila mara.

Katika ukurasa wa 31 wa *Nimefufuka*, mwandishi anatumia methali kuonyesha Upendo akimshauri Chaurembo kwa kutumia methali na anasema:

> Kuteleza si kuanguka. Usiogope ndoa ya pili eti kwa sababu ya kwanza iligonga mwamba. Una haki ya kupenda na kupendwa. Ndoa itakuondolea upweke. (Uku 31)

Kisha chini tu ya maelezo haya mwandishi anatumia picha kuonyesha Chaurembo akitembea kuelekea katika nyumba yake mpya ishara kuwa ametii mashauri ya Upendo shangazi yake. Kwa njia hii ameweka matumizi ya methali hiyo kuwa wazi.




**Picha 8: Chaurembo Akilelekea katika Nyumba Yake Mpya - *Nimefufuka* (Ukurasa 31)**

**Picha na Taswira**

Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Kulingana na Wamitila (2003), taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Wamitila (2011) naye anasema kuwa taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi na picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazotumia. Sababu ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani. Msanii hutumia maelezo ambayo huweza kufanya hadhira ipate aina tofautitofauti za hisi kama hisi za kunusa, kusikia, kuona, kuonja, na hata kugusa. Matokeo ya mbinu hii ni kugusa hisia za msomaji na kumfanya azame katika usomaji. Katika kazi za watoto tulizochunguza picha zimetumiwa kwa njia ya kwamba kwanza mwandishi anaeleza jambo fulani kisha anatumia picha ili kusisitiza jambo hilo. Kwa mfano katika ukurasa wa 18 katika *Sitaki Iwe Siri* mwandishi anatoa maelezo kuhusu Mwalimu Selemani kwa kusema:

> Mwalimu Selemani alikuwa mnene, mweusi na mwenye upara kichwani. Alikuwa mcheshi sana. (Uku 18)

Kisha kuna picha chini ya maelezo haya ikionyesha mwonekano wa Mwalimu Selemani jinsi alivyo mnene, ucheshi wake na tabasamu ya wanafunzi wake. Maelezo ya kitaswira na picha iliyo chini yake yanachangiana kwani maelezo hayo ni kama yanatokana na picha hiyo kabisa.




**Picha 9: Watoto Wakishauriwa na Mwalimu Wao - *Sitaki Iwe Siri* (Ukurasa 18)**

Hali hii pia imetumiwa katika *Nimefufuka* katika ukurasa wa 12 ambapo mwandishi anasema kuhusu mtoto Taabu anayebadilishiwa jina na kuwa Shujaa:

> Polepole anageuka mtoto badala ya kitoto. Afya yake imeanza kuimarika na uzito wa mwili kuongezeka. Licha ya hayo sura yake isiyo ya kawaida huku kwetu, yavutia. Kinapenda kuchezacheza na mwanasesere wake. Kuchekacheka kila wakati. Tabasamu imekijaa na kinafurahia chupa ya maziwa. (Uku 12)

Kisha kuna picha inayodhihirisha hili katika ukurasa wa 13.




**Picha 10: Mtoto Tabu Akicheza na Mwanasesere Wake - *Nimefufuka* (Ukurasa 12)**

Kutokana na yaliyobainika katika makala haya, imekuwa wazi kuwa vipengele vya fani kama tashbihi, nahau, taswira, methali na misemo vinaingiliana na kuchangiana na kipengele cha picha ili kufanya fasihi ya watoto ieleweke kwa urahisi na kufanya ujumbe wake kutosahaulika kwa urahisi. Kwa sababu ya umuhimu huu tungependa kupendekeza kwamba waandishi wa fasihi ya watoto kuhusisha zaidi picha katika kazi za fasihi ya watoto ili kuwafaa zaidi walengwa. Vilevile vipengele vingine vya fani vitumiwe kwa kuingiliana ili kuwezesha uwelewa zaidi katika fasihi hasa ya watoto.

## Hitimisho

Katika makala haya, imebainika kuwa kuna mwingiliano mkubwa wa picha na vipengele vingine vya fani katika fasihi ya watoto. Aidha, picha kama fani zimetumiwa kusisitiza maelezo na ujumbe wa mwandishi katika kazi za fasihi na vilevile kujalizana na fani nyingine kwa kuweka ujumbe katika maneno mengine kwa lengo la kusisitiza. Pia, picha huongeza mambo mengine ambayo hayajatokezwa wazi zaidi katika vipengele vingine vya fani wala katika maelezo yaliyotumiwa. Hatimaye picha huchochea watoto kusoma vitabu vya fasihi walivyoandikiwa, kuteka nadhari yao, kudokeza maudhui katika hadithi husika kwa uwazi, husaidia katika kumbukumbu na kumwezesha mtoto kupokea mambo mengi kwa wakati mmoja.

## Marejeleo


Anderson, N. A. (2006). *Elementary Childrens Literature: The Basics for Teachers and Parents.* Pearson A and B. The University of Virginia.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto.* Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Cass, J. E. (1967). *Literature and the Young Child.* London: Longman Group Ltd.

Davies, A. (1973). *Literature for Children.* Portsmouth: Open University Press.

Hunt, P. (1994). *An Introduction to Childrens Literature.* Oxford: Oxford University Press.

Mbatia, M. (2001). Kamusi ya Fasihi. Nairobi: Standard Textbook, Graphics and Publishind Ltd.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*: Katika Mulika 21. TUKI. Dar es Salaam.

Namanya, E. (2015). *Dhima ya misemo na nahau katika jamii ya wakiga wilayani Kabale Kusini Magharibi mwa Uganda.* Masters Thesis. Pwani University.

Ngugi, P. M. (1997). Childrens Literature Research in Kenyan Universities: Where Are We? *In International Journal of Arts and Commerce.* Vol 1 No. 2Pages 219-229.

Ngugi, P. M. (2011). *"Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya"* katika *Kioo cha Lugha*, juz. 9 kur 84-94.

Njagi, G. M. (2002). *Introduction to the Study of Literature.* Nairobi: Kenyatta University Press.

Norton, D. na Norton, S. (2010). *Through the eyes of a child: An introduction to Childrens Literature (8th ed.)*. Boston, MA: Prentice-Hall.

Odaga, A. B. (1985). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Pearson, L. (2012). *Childrens and Young Adult Literature Database*—Access Card, 1/E.

Saluhaya, M. C. (2013), *Kamusi Elezo Huru*. Wikipedia.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam. KAUTTU LTD.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la 2). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Vuuren, K. (1994). *Astudy of Indegenius Childrens Literature in South Africa*. A masters thesis. University of Cape Town.

Wamalwa, S. (2015). *Sifa na Umuhimu wa Fasihi ya Watoto*. Swahilihub. Swamalwa&ke.nationmedia.com

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2003*). Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Toleo la Pili. Nairobi: Focus Books.